

## **TUME YA UTUMISHI WA UMMA KUBOresha ZAIDI UTOAJI WA HUDUMA KWA WATANZANIA.**

### ***Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma.***

Tume ya Utumishi wa Umma inatarajia kuongeza maarifa na ujuzi katika utunzaji wa kumbukumbu za Ofisi na utekelezaji wa mfumo wa wazi wa mapitio na tathimini ya utendaji wa kazi (OPRAS) baada ya mafunzo ya utunzaji wa kumbukumbu za ofisi na OPRAS kukamilika 5/2/2010.

Mafunzo hayo ambayo yalifunguliwa na Bibi Thecla W. Shangali, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma 1/2/2010 yanasimamiwa na Tume ya Utumishi wa Umma na kuendeshwa na Chuo cha Utumishi wa Umma, Magogoni, Jijini Dar es Salaam.

Wanaoshiriki mafunzo ya utunzaji wa kumbukumbu na OPRAS niwatunza kumbukumbu wasaidizi na Makatibu Mahsusi walioko katika Ofisi za Mikoa na Wilaya za Tume ya Utumishi wa Umma.

Katika Hotuba yake ya ufunguziwa mafunzo, Bibi Thecla Shangali amebaini upungufu uliokuwepo katika utendaji wa kazi kwa Watunza kumbukumbu na Makatibu Mahsusikuwa ni pamoja na uelewa mdogo wa ufunguaji wa mafaili na namna ya kuendesha ofisi.

Kufuatia hali hiyo Tume ya Utumishi wa Umma imeamua kutoa mafunzo kwa makundi yaliyotajwa hapo juu ili kuwaongezea ujuzi katika utendaji wa kazi, hivyo kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma kwa Watanzania kama Bibi Shangali anavyobainisha katika hotuba yake: "Utumishi wa Umma unabadilika na kwenda na wakati, ili mabadiliko hayo yafanikiwe wanatakiwa wawepo watumishi wanaojituma, wenye uelewa wa kazi ambao wako tayari kutekeleza kazi zao ili ili kuweza kutoa matokeo yanayopimika kwa njia ya wazi na kuongeza tija katika Utumishi wa Umma."

Aidha Bibi Shangali amewataka watumishi pia kuwa mfano wa kuigwa katika utendaji wa kazi katika Utumishi wa Umma na kuchukua tahadhali za kujikinga na janga la VVU/ AIDS na kupima HIV/AIDS ili kuweza kupanga mipango ya kazi na maisha.

Mafunzo ya utunzaji wa kumbukumbu na OPRAS yamehudhuriwa na watumishi kutokamikoa ya Dodoma, Dar es Salaam, Kagera, Pwani, Mbeya, Kilimanjaro, Mwanza, Kigoma, Morogoro, Lindi, Tabora, Shinyanga, Rukwa, Mtwara, Tanga, Mara na Arusha.

***Iwapo una maoni/ maswali tafadhali tuandikie:***

Katibu

Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma,

S. L. P 9143

**DAR ES SALAAM.**